



HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI

TAARIFA YA KIKAO CHA KAMATI YA MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MIAKA 60 YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA K KILICHO FANYIKA KATIKA UKUMBI WA MKUU WA WILAYA TAREHE 17/04/2024.

A: MPANGILIO WA MATUKIO.

N a	TUKIO	TAREHE	ENEO	MAHITAJI	MHUSIKA	MAELEZO	MAONI YA KAMATI
1	Kupanda miti	19/04/2024	- Taifa road hadi polisi stesheni(Barabar a mpya inayo tengenezwa) -Rwiza road (Kuelekea kwenye nyumba ya DED na nyuma ya kituo cha polisi) - Chuo cha VETA Uyui -Idete sekondari - Ilalwansimba shule ya Msingi	- Miti - Majembe	-TFS -Maliasili (Kisoma)	-Shughuli hii ya upandaji miti itahusisha na wanafunzi wa Idete na Ilalwansimba hivyo Maafisa elimu Msingi na Sekondari wameagizwa na kamati kuwaandaa wakuu wa shule husika. - Kwa maeneo ya shule,vyuo na taasisi zingine TFS watawagawia miti wakapande kwenye maeneo yao. - AMCOS ziagizwe kupanda miti na kutuma picha za matukio kwa Afisa Ushirika ili kuziunganisha kwenye taarifa	-Haihitaji fedha.

2	Usafi wa mazingira	18/04/2024	-Kuwajibisha Maafisa watendaji kata wote ndani ya Wilaya kufanya shughuli za usafi katika maeneo yao na matukio na picha zitumwe kwa Afisa utumishi kwa ajili ya kuunganisha kwenye taarifa. -Watumishi siku ya alhamisi muda wa masaa mawili kuanzia saa mbili wafanye usafi wa kawaida kuzunguka maeneo ya ofisi	- Vifaa vya usafi	-Afisa Utumishi	-Shughuli hii inaweza ikafanyika maeneo ya ofisini tu na maeneo ya karibu	- Haihitaji fedha
		20/04/2024	-Ilalwansimba senta	-Vifaa vya usafi	- Afisa utumishi - Watumishi wote - Wananchi wa Ilalwansimba - WEO Isikizya - VEO Ilalwansimba - AMCOS	-Wananchi wahamasishwe na wafahamishwe juu ya kufanya usafi wa pamoja siku ya Jumamosi kuanzia saa 2:00-4:00 Asubuhi. - Wafanya biashara wafunge maduka kwa muda ili kuungana kwenye zoezi la usafi.	-Haihitaji fedha
3	Michezo,Sanaa,Utamaduni	19/04/2024	-Kwenye uwanja wa shule ya	-Mipira -Jezi	-WEO -Keegan	-Kutakuwa na ligi ya mpira wa miguu itakayo	-Fedha zinahitajika

			msingi ilalwansimba		- A/Tarafa -Maafisa Elimu Msingi na Sekondari	shirikisha timu 4 ambazo ni Umoja Isikizya,Nsaguzi,Ilalwansi mba na Igoko (Zawadi iwe mbuzi mkubwa kwa mshindi wa kwanza na mbuzi mdogo kwa mshindi wa pili),fainali iwe tarehe 24/04/2024	kwa ajili ya zawadi kwa washindi
						-Ngoma za asili watumike wanafunzi shule za ilalwansimba na idete kwani huwa wanakuwa nazo.	-Haihitaji fedha
						-Insha maafisa elimu kuwajulisha walimu wa idete na Ilalwansimba kulisimamia zoezi hilo na insha zizingatie kauli mbiu,Washindi wawili kutoka sekondari na wawili kutoka shule ya msingi wakabidhiwe zawadi zao siku ya kilele na Mhe.Mkuu wa Wilaya	-Fedha inahitajika kwa washindi wa insha
						-Wasanii,vikundi au mtubinafsi mwenye burudani yoyote inayo lenga ujumbe wa siku husika wakaribishwe ila hakuta kuwa na malipo yoyote	-Fedha haihitajiki
						-Matangazo yatumie PA gari izunguke maeneo ya jirani kwa ajili ya kuwatangazia wananchi na muziki na vipaza sauti vikodiwe viwepo kwenye matukio haya muhimu	-Zinahitajika fedha

						kwani kutakuwa na watu wengi hivyo bila vipaza sauti ujumbe hautasikika	
4	Mapambo	18/04/2024	-Ofisi ya DC -Ofisi ya DED -Kwenye kona ya barabara za kuingia kwa DED na DC -Kwenye nguzo za taa barabarani -Kwenye taasisi za serikali zote	-Mapambo -Mpambaji -Vipeperushi	-DCDO -A/Tarafa	-Mpamabaji atafutwe mapema ili atoe gharama zake za upamabaji ili mchakato wa malipo uanze mapema na upambaji uanze siku ya Alhamisi ya tarehe 18/04/2024	-Zinahitajika fedha
5	Maombi na dua	22/04/2024	-Ofisi ya DED kwa nje	-Viongozi wa dini (BAKWATA, CCT, TEC na Potestant) - Vipaza si	-A/Tarafa -WEO	-Maombi yatafanyika nje ya ofisi ya DED	-Zinahitajika fedha kwa ajili ya vipaza sauti
6	Tamasha la muziki	25/04/2024	-Ukumbi mkubwa wa DC	-Viti -TV/Projector -Wasanii -Chakula	-A/Tarafa -DCDO -Utumishi -WEO	-Washiriki wote wanatakiwa kuwepo kuanzia saa 10:00 Jioni ya mpaka saa 3:00 usiku wakati wa kusikiliza hotuba	-Zinahitajika fedha kwa ajili ya chakula cha jioni/usiku

WASHIRIKI.

-Viongozi wa dini, Viongozi wa kisiasa, Wazee maarufu, watumishi wote, na wananchi wote